

BARAZA LA FAMASI



UTARATIBU WA KUHUISHA VIBALI VYA FAMASI KWA MFUMO WA KILEKTRONIKI

UTANGULIZI

1. **DHUMUNI:** Kutekeleza takwa la Kifungu Na. 36 cha Sheria ya Famasi, Sura 311 (*The Pharmacy Act, Cap 311*).
2. **WAHUSIKA:**
 - Wafamasia wasimamizi wa famasi husika; na
 - Fundi Dawa Sanifu.
3. **MFUMO WA UHUISHAJI:** Mfumo wa Kieletroniki utakaomuwezesha Mfamasia Msimamizi au Fundi Dawa Sanifu kuhuisha taarifa na kibali cha jengo husika analosimamia kwa mwaka wa fedha 2022/23. Mfumo unapatikana kwa kubofya kiunganishi hapa chini <https://www.pc.go.tz/applications/permitapplication.php>

LENGO

Kuboresha ufanisi wa uhuishaji wa vibali na uwasilishaji wa taarifa kutoka kwa wasimamizi. Aidha, mfumo utaokoa muda wa uhuishaji na upatikanaji wa vibali kwa wakati.

UTARATIBU WA KUHUISHA KIBALI CHA KUTOA HUDUMA YA DAWA KWENYE REJESTA

- a) **FOMU YA KIELEKTRONIKI:** Mfamasia ANAYESIMAMIA FAMASI au Fundi Dawa Sanifu anayesimamia ADDO YA JUMLA (ARW) au GHALA LA DAWA atapashwa kuingia katika akaunti yake aliyofungua awali kwenye kanzidata (*database*) ya Baraza.
- b) **Mhuishaji** Anapaswa kubonyeza kitufe cha kuhuisha na kuingiza taarifa zinazohitajika.
- c) **VIAMBATA: Hakikisha kuwa** nakala zote zinazopashwa kuambathishwa zipo katika Mfumo wa PDF. Nakala za kuambathisha ni kama zifuatazo;
 - ◆ *A current signed contract of agreement of Superintendent pharmacist, P/Technician, P/Assistant, P/Dispenser (period of one year);*
 - ◆ **A declaration form if the owner is also a superintendent;**
 - ◆ *A signed commitment form available in the www.pc.go.tz (instead of commitment letter) of registered, enrolled/enlisted or dispenser pharmaceutical personnel;*
 - ◆ *Memorandum of Understanding (pages that show Directors, identification cards recognized by government for personal identification and their signatures);*
 - ◆ *Tax Identification Number (TIN) Certificate;*
 - ◆ *Business Name Registration Certificate from BRELA;*
- d) Taarifa zote zitakazokuwa zimewasilishwa na mfamasia msimamizi endapo zitakuwa si halali, mfamasia husika atachukuliwa hatua za kisheria.
- e) Baada ya kukamilisha ujazaji wa taarifa, mfumo utakupatia NAMBA YA MALIPO (*Control Number*) ya kulipia kibali ambayo itatumwa kwenye namba ya simu uliyoiingiza.
- f) **KUKAMILISHA UHAKIKI:**

Baada ya uwasilishaji wa taarifa za uhuishaji, uhakiki utafanyika na utakapokamilika utapokea ujumbe wa sms wa kukujulisha upatikanaji wa kibali husika.

Mfamasia/Fundi Dawa Sanifu atawajibika kurudi kwenye akaunti yake kwa ajili ya kudurufu (*printing*) kibali cha duka husika.

- g) **ADA:** Malipo ya ada ya kuhuisha kibali cha biashara kwa mujibu wa Kanuni za Ada na Tozo ya Mwaka 2012 ni kama ifuatavyo:-

Na.	Aina ya Biashara	Ada ya Kibali	Ada ya Taaluma	Jumla
1.	Rejareja	TZS 200,000/=	TZS 200,000/=	TZS 400,000/=
2.	Jumla	TZS 350,000/=	TZS 500,000/=	TZS 850,000/=
3.	Jumla na Rejareja	TZS 550,000/=	TZS 700,000/=	TZS 1,250,000/=
4.	Ghala	TZS 100,000/=	NIL	TZS 100,000/=
5.	Duka la Jumla la ADDO	TZS 200,000/=	TZS 200,000/=	TZS 400,000/=

- h) **MUDA WA MALIPO:** Zoezi la kuhisha kwa mwaka wa fedha **2022/2023** litaanza rasmi tarehe **01 Julai 2022** mpaka **31 Julai 2022** ambapo baada ya tarehe **31 Julai 2022** utalazimika kulipa pamoja na **faini ya 25%** ya kiwango ulichopaswa kulipia.

NAMBA ZA SIMU KWA MSAADA:

Na	Ofisi za Baraza la Famasi	Namba ya simu
1.	Kanda ya kati na magharibi (Dodoma · Singida · Tabora · Kigoma · Iringa)	0736 222 527
2.	Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam · Lindi · Morogoro · Mtwara · Pwani)	0736 222 523
3.	Kanda ya nyanda za juu kaskazini (Arusha · Kilimanjaro · Manyara · Tanga)	0736 222 531
4.	Kanda ya nyanda za juu kusini (Mbeya · Njombe · Rukwa · Ruvuma · Songwe · Katavi)	0736 222 521
5.	Kanda ya ziwa (Geita · Kagera · Mara · Mwanza · Shinyanga · Simiyu)	0736 222 501
6.	Makao makuu, Dodoma	0736 222 516

Imetolewa na:
Msajili,
Baraza la Famasi
S.L.P. 1277,
Bila malipo 0800110015
Dodoma